

## **Kampeni ya CPJ ya #WhereIsAzory kuangazia kutoweka kwa mwandishi wa Tanzania**

New York, Aprili 4, 2019—Kamati ya Kuwalinda Wanahabari (CPJ) leo imezindua kampeni ya #WhereIsAzory kukumbushia kesi ya mwandishi wa habari wa kujitegemea Mtanzania [Azory Gwanda](#), ambapo kesho zitatimia siku 500 toka alipoonekana mara ya mwisho.

[Kampeni inalenga](#) kuhamasisha, kujenga uelewa kuhusu Gwanda, na kuzitaka mamlaka za Tanzania kufanya uchunguzi wa kuaminika na kuweka bayana hatima yake. Watu wanaweza kushiriki katika kampeni kwa kutumia hashtag #WhereIsAzory na #MrudisheniAzory katika mitandao ya kijamii.

“Azory Gwanda ni mwandishi wa habari wa kujitegemea aliyekuwa akiandika kuhusu jamii yake na kamwe hapaswi kuwa takwimu nyingine tu,” anasema Angela Quintal, mratibu wa CPJ Afrika. “Kupitia kampeni hii tunataka kuhakikisha kwamba kesi ya Gwanda inapewa kipaumbele na mamlaka za Tanzania na kupata majibu yanayohitajika kuhusu kile hasa kilichompata. Mpaka wakati huo, waandishi wa Tanzania hawawezi kujisikia wako salama.”

Mara ya mwisho Gwanda kuonana na familia yake na rafiki zake ilikuwa Novemba 21, 2017, kwa mujibu wa [utafiti wa CPJ](#). Gwanda alimuambia mkewe, Anna Pinoni, kwamba ana safari ya dharura na angerejea siku inayofuata. Hajaonekana tangu siku hiyo.

Katika mahojiano na gazeti la *Mwananchi*, Pinoni [alisema](#) anadhani kupotea kwa mume wake kunaweza kuhusishwa na kazi yake ya [kuripoti](#) juu ya mfululizo wa mauaji ya ajabu yaliyokuwa yakitokea katika mkoa wa Pwani nchini Tanzania, maoni yanayoshikiliwa na wengine ambao CPJ iliongea nao.

Nchini Tanzania, waandishi wa habari na vyombo vya habari wanachukua tahadhari kwa kuhofia yanayoweza kuwakuta iwapo watapaza sauti kuhusu kesi ya Gwanda. Wakati wawakilishi wawili wa CPJ waliposhikiliwa kwa usiku mmoja na kuhojiwa nchini Tanzania mwaka uliopita, [waliulizwa](#) juu ya maslahi yao katika kisa cha Gwanda. Kupotea kwake kunakuja huku kukiwa na [kuzorota kwa uhuru wa vyombo vya habari nchini](#), ikiwa ni pamoja na maagizo ya serikali kufungia baadhi ya vyombo vya habari, faini, kanuni zenye vizuizi na kukamatwa hovy kwa waandishi wa habari.

CPJ Afrika itaangazia kesi ya Gwanda katika [Twitter](#), [Facebook](#), na [Instagram](#).

###

CPJ ni kamati huru, isiyojiendesha kwa faida inayofanya kazi kulinda uhuru wa wanahabari duniani kote. Mawasiliano kwa Vyombo vya Habari:

Bebe Santa-Wood

[press@cpj.org](mailto:press@cpj.org)